*Tangazo la Serikali Na. 528 (Inaendelea)*

**TANGAZO LA SERIKALI Na. 528 la Tarehe 10/07/2020**

# SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

## (SURA YA 290)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(i))*

## SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO YA UVUVI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI ZA MWAKA 2020

**Jina na Tarehe ya kuanza kutumika**

**1.** Sheria hizi zitaitwa **Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Uvuvi) za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi za mwaka 2020** na zitaanza kutumika mara zitakapo tangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**Eneo la Matumizi**

**2.** Sheria Ndogo hizi zitaztumika katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

**Tafsiri**

**3.** Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama tafsiri itafafanua vinginevyo:

**"Afisa Mwidhiniwa"** maana yake ni Afisa Uvuvi aliye au asiye na taaluma ya Uvuvi au Afisa au Mtumishi yeyote anayeruhusiwa au kuteuliwa na Mkurugenzi kwa maandishi kutekeleza wajibu wowote kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

**"Afisa Uvuvi"** maana yake ni Mtumishi wa Serikali aliye chini ya Utumishi wa Halmashauri katika Sekta au Idara ya Uvuvi mwenye kuanzia cheo cha Mvuvi Msaidizi;

**"Baruti"** maana yake ni bomu au mlipuko wa bomu ambao unasababisha uharibifu wa mazingira na papo hapo kuua

viumbe, samaki na mazalia yao kwenye sehemu ya mlipuko huo;

**"Bwawa"** maana yake ni bwawa la Nyumba ya Mungu.

**"Chombo cha Uchukuzi"** maana yake ni chombo chochote cha usafiri wa majini au nchi kavu kilichotengenezwa maalum kwa kutumika kubeba, kusafirisha au kuchukua samaki wakavu, wabichi kwa kutumia vibebea barafu (Ice Box Containers) na chombo hiki chaweza kuwa gari, boti, karua, kilagala, ngama, mashua ya kutumia injini, mashua, mtumbwi wa kutumia joshi au kasia;

Kwa chombo kilichosajiriwa kwa ajili ya kubeba abiria sharti lake ni lazima kiwe kimesajiliwa na SUMATRA.

**"Chombo cha uvuvi"** maana yake ni chombo chochote kilichoandikishwa au kutoandikishwa na kilichokatiwa au kutokatiwa leseni ya uvuvi chini ya Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2002, Kanuni zake za 2009 pamoja na marekebisho ya Sheria ya Uvuvi Na.22/2003;

**"Dandali"** maana yake ni vipande viwili vya fito vilivyotengenezwa kwa duara au namna nyingine yoyote na kusukwa kwa kamba na miti,katani au manila na hutumika kufungia samaki wakavu wakati wa kusafirisha kwenda kuwauza;

**"Eneo la Kuanika Samaki"** maana yake ni eneo la ardhi lililotengwa na Serikali au jamii la ufukweni mwa Bwawa (Mwaloni) lenye urefu wa mita zipatazo sitini kutoka ufukweni hadi nchi kavu lenye mchanga au nyasi fupi fupi linalotumiwa na wavuvi kuanika samaki;

**"Gunia"** maana yake ni mfuko mkubwa uliotengenezwa kwa kamba za katani, nailoni, polythene au viroba kwa madhumuni ya kuchukulia samaki au dagaa na kutumika kufungia samaki wakavu au wabichi wakati wa kuwasafirisha;

**“Halmashauri”** Maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Moshi;

**“Kutengeneza Samaki”** maana yake ni kukata katika vipande vipande visivyo au vyenye mifupa, kuweka barafu, kufukiza, kuhifadhi au kukausha kwa kutumia chumvi (kayabo), kukaanga au kuhifadhi samaki kwa njia au namna yoyote ile kwa madhumuni ya biashara;

**“Kuuza nje”** maana yake ni kutoa bidhaa zitokanazo na uvuvi na mazao yake katika Halmashauri ya Moshi na kupeleka mahali popote nje ya eneo la Mamlaka ya Halmashauri’

**“Mchuuzi wa Samaki”** maana yake ni Mtu binafsi, kikundi cha watu, Taasisi, Kampuni, Shirika au Chama kinachojihusisha au kushughulika na biashara ya samaki au bidhaa yoyote kwa kununua, kuuza kutengeneza au kusafirisha samaki hao au mazao yake kwa kuzingatia kanuni kuu za uvuvi za mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake;

**“Mkurugenzi “** maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi au Mtu yeyote aliyeteuliwa kukaimu nafasi hiyo pamoja na kutekeleza majukumu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

**“Mvuvi”** maana yake ni mtu,kikundi cha watu,Taasisi au Shirika linalojishughulisha na shughuli za uvuvi Wilayani Moshi;

**“Mwalo”** maana yake ni kando kando ya bwawa au sehemu yoyote ile inayotumiwa na wavuvi kutua, kupakua au kupakia samaki na zana za uvuvi na bidhaa nyinginezo kwa madhumuni ya biashara au matumizi ya nyumbani;

**“Sheria”** ina maana ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Na.9 ya 1982 pamoja na marekebisho yake;

**"Sumu"** maana yake ni dawa zitokanazo na miti aina ya mruku au mti wowote ule ambao majani yake, magome au mizizi ya miti hiyo iliyopondwa pondwa na kutengenezwa madawa ya kienyeji au dawa inayotokana na kemikali za viwanda ambayo hutumika kwa kuwalewesha au kuwaua samaki na zenye madhara kwa binadamu;

**"Tenga"** maana yake ni chombo ambacho kimetengenezwa kwa mianzi au matete ambacho kinatumika kusafirishia bidhaa za mazao ya uvuvi.

Tenga nne ni sawa na dandali moja kwa maana ya tafsiri ya utozaji ushuru wa Halmashauri.

**"Wakala"** maana yake ni mtu,Taasisi,Kampuni au mtu aliyepewa uwakala wa kukusanya ushuru wa samaki na Halmashauri na hii itahusisha pia Watumishi wa Wakala huyo waliopewa vitambulisho vilivyosainiwa na Mkurugenzi vyenye kuonyesha aina ya uwakala na mwaka walioruhusiwa kukusanya ushuru huo;

**"Waziri"** ina maana ya Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mita;

**Ushuru wa mazao yanayotokana na uvuvi**

**4.** Halmashauri itatoza ushuru kwa mazao yanayotokana na uvuvi ndani ya Wilaya kama ilivyobainishwa katika jedwali "A" la Sheria Ndogo hizi.

Vile vile mazao ya uvuvi yaliyoingizwa ndani ya Halmashauri kwa madhumuni ya biashara na hayakulipiwa ushuru yatalipiwa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

**Kibali**

**5.** (i) Itakuwa ni wajibu wa kila Kampuni, Mtu au Watu wanayojishughulisha na ukusanyaji au ununuaji wa samaki au mazao yake kwa kutumia, gari, mtumbwi, karua au ngama au chombo kingine chochote cha kusafirisha samaki na mazao yake ndani ya eneo la Halmashauri kuhakikisha kwamba inaomba kibali na kupata kibali cha Halmashauri.

*Tangazo la Serikali Na. 528 (Inaendelea)*

(ii) Mtu binafsi mwenye lengo la kukusanya ushuru wa Samaki kwenye Halmashauri kwa kutumia mashua, mtumbwi, karua, ngama, gari au kwa kutumia sanduku la kuhifadhia samaki (Thermo Box) atatakiwa kutuma maombi kwa Mkurugenzi akionesha aina ya chombo atakachotumia kukusanyia na kusafirishia samaki na maombi yake yakipokelewa na kukubaliwa atapaswa kusaini mkataba wa kulipa ushuru wa samaki kwa Halmashauri kama ulivyobainishwa katika jedwali “A” la Sheria Ndogo hizi.

(iii) Kampuni, Mtu au Taasisi ambayo imekubaliwa maombi yake atapewa kibali na Halmashauri ambayo imebainishwa katika jedwali la pili

(iv) Kila Taasisi, Mamlaka, Mtu, Kikundi cha watu au Kampuni inayotumia au kumiliki chombo cha uvuvi ndani na nje ya eneo la Halmashauri itawajibika kulipa ushuru wa samaki kwa viwango vilivyobainishwa katka jedwali “A”la Sheria Ndogo hizi.

(v) Ushuru wa Samaki utakusanywa na Afisa Uvuvi, Afisa Mwidhiniwa, Mkusanya Ushuru au Wakala wa Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(vi) Kila mwenye kumiliki chombo cha uvuvi, Mtumishi au Msimamizi wake aliyemteua atapaswa kutoa ushirikiano kwa Afisa Uvuvi, Afisa Mwidhiniwa, Mkusanya Ushuru au Wakala wa Halmashauri kuhakikisha kuwa ushuru wa samaki unalipwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(vii) Ushuru wa samaki na mazao yake hautatozwa mara mbili kwa samaki au bidhaa iliyokwisha kulipiwa ushuru wa Halmashauri sehemu nyingine ndani ya Halmashauri ya Moshi; isipokuwa atapaswa kuonyesha stakabadhi ya ushuru aliyolipia kutoka sehemu aliyolipia samaki au bidhaa yake ndani ya eneo la

Halmashauri ya Moshi kwa ajili ya uhakiki au ukaguzi.

**Makosa** **6.** Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi itakuwa ni kosa kwa:-

(i) Mtu kutoka nje ya eneo la Halmashauri kufanya shughuli za uvuvi bila kuripoti kwa wasimamizi wa rasilimali za uvuvi (BMU) na kupata kibali kilichobainishwa katika jedwali "B" la Sheria Ndogo hizi kinachohusu kufanya shughuli za uvuvi ndani ya eneo la Halmashauri.

(ii) Kampuni Taasisi au Mtu Binafsi kufanya shughuli za ukusanyaji, utengenezaji na usafirishaji wa samaki wabichi, wakubanikwa kwa moshi, jua au chumvi (Kayabo) bila ya kuwa na kibali cha Mkurugenzi au Afisa uvuvi kinachomruhusu mtu kufanya biashara hiyo au kusafirisha samaki au bidhaa zake nje ya Halmashauri bila ya kuwa na kibali husika kama kilivyobainishwa katika jedwali "C". Kibali hicho kitalipiwa na muhusika atapatiwa risiti ya Halmashauri;

(iii) Mmiliki, Msimamizi au mwenye chombo cha uchukuzi kupakia au kusafirisha mzigo wowote wa samaki, mabondo au bidhaa nyinginezo zitokanazo na samaki toka kwenye mwalo au eneo la Halmashauri kabla ya kulipiwa ushuru wa Halmashauri kwa viwango vilivyobainishwa katika jedwali "A" la Sheria Ndogo hizi;

(iv) Kampuni, Taasisi, Mtu au kikundi cha watu kuvua samaki kwa kutumia nyavu za makila (Gillnets) chini ya ukubwa wa macho (mech size) ya inchi 3 au nyavu zozote zile zilizokatazwa na Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake za 2009 pamoja na marekebisho yake isipokuwa kwa mitego migono, madema na ndoano;

(v) Kuvua au kuua samaki wadogo ambao hawajakua kufikia kiwango cha kuvuliwa;

(vi) Kufanya shughuli za uvuvi na kusafirisha samaki nyakati za usiku bila ya kulipia ushuru;

(vii) Kumzuia, kumgomea au kumshambulia Afisa Uvuvi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala wakati anapotekeleza mojawapo ya majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(viii) Kufanya biashara ya uvuvi au kuuza samaki au mazao yatokanayo na samaki bila leseni.

(viii) Kusafirisha samaki (wabichi) ambao watathibitika wana madhara kwa mlaji.

(ix) Kulima mazao ya chakula ndani ya bwawa na matumizi ya viatilifu ( Sumu za Magugu na Wadudu), kuchunga mifugo na kujenga nyumba na kuishi ndani ya eneo la hifadhi ya bwawa.

(x) Kuuza samaki wabichi na wakavu katika maeneo yasiyostahiki kama barabarani bila kujali afya ya mlaji.

**Muda wa kusimamisha Shughuli za Uvuvi.**

**7.** Kutakuwa na kipindi ambacho shughuli za uvuvi zitasimama ili kupisha samaki kuzaliana, kipindi hicho kitakuwa kinatangazwa na Halmashauri.

Mtu yeyote hatoruhusiwa kuvua samaki katika kipindi ambacho shughuli za uvuvi zitakuwa zimezuiliwa.

**Ushuru**

**8.** Mazao ya samaki ambayo yatakuwa hayajalipiwa ushuru, hayataruhusiwa kusafirishwa kutoka eneo la Halmashauri bila kuwa yamelipiwa ushuru na kuwa na kibali endapo kutakuwa na ukaidi, mhusika atatakiwa kulipa ushuru anaodaiwa pamoja na asilimia hamsini ya anachodaiwa ikiwa ni kufidia gharama za kufuatilia ushuru huo.

**Sehemu zisizo ruhusiwa kuuza,**

**9.** Mtu yeyote, Taasisi, Mamlaka,Kampuni, Mfanyabiashara au Mvuvi atakayepuuza au kukataa kununua au kusafirisha samaki kwa kutumia sehemu nyingine zisizoruhusiwa kwa

**kusafirisha na kununua mazao ya uvuvi**

mujibu wa Sheria Ndogo hizi

**Usajili wa Vyombo vya uvuvi**

**10.** Vyombo vya uvuvi vinatakiwa kuwa vimesajiliwa na Halmashauri na mara ambapo chombo hakitakuwa kimesajiliwa mmiliki wa chombo husika atatakiwa kukisajili na kulipia faini ya asilimia hamsini ya ushuru ili kufidia gharama za ufuatiliaji na endapo atakuwa ameshindwa kulipia chombo chake ndani ya saa ishirini na nne, Halmashauri au Wakala atataifisha chombo husika na kukiuza kwa mnada kufidia gharama pamoja na ushuru.

**Marufuku ya kutojirudia kwa Namba ya usajili.**

**11.** Chombo cha uvuvi hakitatakiwa kujirudia namba ya usajili na itakapobainika kuwa chombo au vyombo vya uvuvi au usafiri wa majini kimejirudia namba ya usajili Halmashauri itataifisha vyombo vyote ambavyo vimejirudia namba na itaviuza kwa mnada wa hadhara.

**Ada ya Kibali**

**12.** Kibali cha kusafirishia mazao ya uvuvi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kitalipiwa shilingi 10,000/=

**Adhabu**

**13.** Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakua ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua laki mbili(200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kutumikia kifungo kisichopungua mwaka mmoja (1) na kisichozidi miaka miwili (2) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

**Kufifilisha Kosa**

**14** Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa endapo mtu atakiri kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kwa kumtoza kiasi kisicho pungua shilingi laki mbili na isiyozidi million moja baada ya kujaza fomu maalum iliyoambatishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

***Tangazo la Serikali Na. 528 (Inaendelea)***

## JEDWALI LA KWANZA

## SEHEMU "A"

**(*Limetungwa Chini ya Kifungu Cha 4 Na 5*)**

| MAZAO YA UVUVI | UJAZO | KIASI CHA USHURU<br>Tshs |
|---|---|---|
| **Perege**<br>**Kambale** | **Kilo 11-20**<br>**Kilo 21-60**<br>**Kilo 61-100** | **1000/=**<br>**2000/=**<br>**6000/=** |
| **Dagaa (ila si za kutoka Bwawa la Nyumba ya Mungu)** | **Gunia la ndoo 10 za lita ishirini.** | **10,000/=** |

## JEDWALI LA PILI

## SEHEMU "A"

***(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 5*)**

Picha ya Muombaji

## KIBALI CHA KUENDESHA SHUGHULI ZA UVUVI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI

Namba ya Leseni………………………

Namba ya Simu……………………….

***Tangazo la Serikali Na. 528 (Inaendelea)***

Kibali hikikinatolewa kwa Bwana/Bibi/Bi./Ndugu…………………………………

Ambaye ni mkazi wa……...…………………Wilaya ya…………………………

Mkoa wa ……………………………………………….kufanya shughuli za uvuvi/ununuzi/

usafirishaji wa Samaki kutoka eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Kibali hiki kitatumika kuanzia tarehe…….mwezi wa ……… Mwaka ………..….

Mpaka tarehe ………………. mwezi……………………… mwaka……………

Mwombaji wa kibali amelipa malipo yote yanayohusiana na kibali hiki kwa stakabadhi

Na……………………………ya tarehe……..mwezi…………….. mwaka……….

**……………………………………………..**

**Afisa Uvuvi (W)**

**SEHEMU "B"**

***(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 5)***

**KIBALI CHA KUSAFIRISHA SAMAKI KUTOKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI**

Kibali kinatolewa kwa Bwana/Bibi/Bi/Ndugu…………………..…..………………

Ambaye anamiliki leseni ya biashara Na……….……………………ya kusafirisha Samaki/Mazao/

***Tangazo la Serikali Na. 528 (Inaendelea)***

Bidhaa zitokanazo na samaki kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwenda sehemu iliyobainishwa hapa chini kwa ajili ya biashara/matumizi ya nyumbani.

| **Na.** | **Aina ya Samaki** | **Idadi ya Mzigo** | **Kizio** | **Thamani yake** | **Kituo anakopeleka** | **Ada iliyolipwa kwa Halmashauri** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |

Tarehe ambayo kibali kimetolewa………..…………………………………………

Tarehe ya mwisho wa kibali…………………………………………….…………

**……………………** **…...…………………**

**Afisa Uvuvi (W)** **Saini ya Mwombaji wa Kibali**

## JEDWALI LA TATU

***(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 14)***

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ..................................................................... nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya......................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwamba tarehe ..........ya Mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …….. cha **Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Uvuvi) za Halmashauri ya Wilaya ya Moshi za mwaka 2020**

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha shilingi laki mbili badala ya kushtakiwa Mahakamani.

*Tangazo la Serikali Na. 528 (Inaendelea)*

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……

**Jina: ....................................................**

**Saini: ...................................................**

Mbele ya**:**

**Jina……...............................................**

**Cheo: .................................................**

**Saini: .................................................**

**Tarehe: ............................................**

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi umebandikwa katika Sheria Ndogo hizi kwa Azimio la kikao cha Halmashauri kilichoitishwa na kufanyika tarehe 29/02/2019 na ilibandikwa mbele ya:

**Kastori G. Msigala**<br>
**MKURUGENZI MTENDAJI**<br>
**HALMASHAURI YA WILAYA MOSHI**

**Mhe. Michael S. Kilawila,**<br>
**MWENYEKITI**<br>
**HALMASHAURI YA WILAYA MOSHI**

**NAKUBALI,**

Dodoma,
**27 Disemba 2019**

**Mhe. Selemani S. Jafo (Mb.),**
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa na Serikali za*
*Mitaa.*